TANGAZO LA SERIKALI NA. 287 La Tarehe 19/3/2021

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA MAMLAKA ZA WILAYA

(SURA YA 287)

# SHERIA NDOGO

*(Imetungwa chini ya kifungu cha 153)*

SHERIA NDOGO YA KUDHIBITI OMBAOMBA YA HALMASHAURI YA WILAYA YA CHUNYA YA MWAKA 2021

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Kudhibiti Ombaomba ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya za Mwaka 2021.

Tafsiri

2. Katika Sheria Ndogo hii isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo:-

“Afisa Mwidhiniwa” maana yake ni afisa yeyote wa Umma atakayeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

“Eneo la Wazi” maana yake ni eneo lolote lenye bustani, au viwanja lisilokuwa eneo la faragha;

“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Chunya;

“Hifadhi isiyo rasmi” maana yake ni mahali popote au eneo ambapo haparuhusiwi watu kukaa, au kuweka makazi;

”Kituo cha Hifadhi”maana yake ni kituo au mahali au jengo lolote ambalo limetengwa au linatumika katika kuwahifadhi ombaomba, Wazee, watoto au walemavu kwa lengo la kuwapatia mahitaji ya msingi;

“Mkazi” maana yake ni mtu yeyote anayeishi au anayefanya shughuli yoyote ndani ya eneo la Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya;

"Mtaa" maana yake ni eneo lolote lililopo ndani ya Halmashauri na inajumuisha maeneo yote ya barabara na hifadhi za barabara na njia ya waenda kwa miguu;

"Ombaomba" maana yake ni mtu yeyote, mwenye ulemavu au asiye na ulemavu anayeishi kwa kutegemea kuombaomba chakula au fedha au vitu vingine kutoka kwa mtu mwingine kwenye Mitaa na maeneo ya wazi yaliyoko ndani ya eneo la Halmashauri.

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi au kikundi cha watu, Kampuni au Shirika ambalo limeteuliwa na Halmashauri kufanya kazi yoyote chini ya Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa kudhibiti ombaomba.

3. (1) Halmashauri itakuwa na wajibu wa kudhibiti ombaomba kwenye eneo lote la Halmashauri.

(2) Halmashauri inaweza kumteua wakala ambaye atatekeleza jukumu la kudhibiti ombaomba kwenye sehemu au eneo lote la Halmashauri kwa niaba ya Halmashauri.

(3) Kila mkazi wa Halmashauri analo jukumu la kudhibiti ombaomba kwenye eneo analoishi kwa kutoa taarifa kwa Mkurugenzi, Afisa Mtendaji wa Kata au Afisa Mtendaji wa Mtaa, au Afisa Mwidhiniwa.

Kumtambua ombaomba

4. (1) Mtu yeyote atakayekutwa mtaani au kwenye eneo la wazi akiomba fedha au chakula kwa mtu au watu wengine atahesabika kuwa ni ombaomba.

(2) Mtu yeyote atakayekutwa au kuonekana akiomba Mitaani au kukaa, kusimama au kulala mitaani au kwenye maeneo ya wazi na kupiga muziki ili kuomba au kuonesha vidonda au ulemavu kwa madhumuni ya kuomba wakati wowote atahesabika kuwa ni ombaomba.

Taratibu za kuwakamata

5. (1) Mtu yeyote atakayekutwa Mtaani au maeneo ya

ombaomba.

wazi akiomba fedha, chakula au kitu kingine chochote, atakamatwa na kuchukuliwa taarifa zake muhimu ikiwemo:-

a) jina lake kamili;

b) jinsi na Umri;

c) kijiji, Wilaya na Mkoa anaotoka;

d) atapigwa picha ili iwe kumbukumbu;

(2) Picha iliyopigwa chini ya kifungu cha 5(1)(d) itatumika kwa matumizi ya ofisi ili kurahisisha utambuzi iwapo atarudia kuombaomba.

(3) Bila ya kuathiri kifungu kidogo cha (1) cha Sheria Ndogo hii, ombaomba aliyekamatwa anaweza kufikishwa mahakamani.

Msaada kwa wenye mahitaji

7. Mtu yeyote, kikundi cha watu au taasisi yeyote inayohitaji kutoa msaada wa aina yoyote ile kwa watu wanaohitaji msaada watatakiwa kuwasilisha misaada hiyo kwenye kituo cha hifadhi, taasisi za dini, vituo vya kulelea watoto yatima, wazee au wenye ulemavu na watu wengine wasiojiweza au Ofisi ya Ustawi wa Jamii ya Halmashauri.

Makosa

8. (1) Itakuwa ni kosa chini ya Sheria Ndogo hii kwa mtu yeyote endapo;

a) ataomba na kupokea msaada wa fedha, chakula au kitu kingine chochote mitaani au kwenye maeneo ya wazi na mahali popote pasiporuhusiwa;

b) atatoa msaada wa fedha au chakula au kitu kingine chochote kwa ombaomba yeyote mtaani au kwenye maeneo ya wazi na mahali popote ambako siyo kituo cha hifadhi;

c) atamtembeza mtu yeoyote awe mzima au mwenye ulemavu kupita barabarani au mitaani au maeneo ya wazi kwa kutumia chombo chochote maalumu cha walemavu au kumtembeza kwa miguu au kwa njia nyingine yoyote kwa lengo la kuombaomba;

d) atamsafirisha kutoka eneo moja hadi jingine mtu yeyote kwa lengo la kumtumia kuombaomba mitaani;

e) atamtumikisha mtoto kwa shughuli za kuomba, kwenye magari, barabarani au mahali pengine popote;

f) atashindwa kutoa taarifa au kutoa taarifa za uongo kuhusiana na ombaomba kwa lengo la kukwamisha upatikanaji wao ili wasiondolewe maeneo yasiyo rasmi;

g) atamzuia Afisa yeyote au wakala kutekeleza majukumu yake yaliyoainishwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Mtu yeyote atakaye kiuka masharti ya kifungu (1) atakuwa ametenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Adhabu

9. Mtu yeyote atakayekiuka au kwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyozidi shilingi laki tatu au kutumikia kifungu kisichozidi miezi kumi na mbili jela au vyote viwili faini na kifungo kwa pamoja.

Uwezo wa kufililisha kosa.

10.- (1) Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufililisha kosa kwa kumtoza faini kiasi kisichozidi shilingi laki mbili na mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii na kukiri kwa maandishi kwa kujaza fomu iliyoambatanishwa katika Jedwali la Sheria Ndogo.

(2). Bila kuathiri kifungu cha (1) cha Sheria Ndogo Hii Halmashauri inaweza kuwarejesha ombaomba wote watakaokamatwa ndani ya maeneo ya Halmashauri kwenye Mikoa wanayotoka na kuwakabidhi kwa Katibu Tawala wa Mkoa huo.

(3) Iwapo ombaomba yeyote aliyefililishiwa kosa lake chini ya Sheria Ndogo hii kwa kutozwa faini au amerejeshwa kwenye Mkoa anaotoka atarudia tena kosa au kurejea tena ndani ya eneo la Halmashauri kwa madhumuni ya kuendelea kuwa ombaomba akikamatwa atafikishwa mahakamani na akitiwa hatiani atahukumiwa na kuadhibiwa kwa mujibu Sheria Ndogo hii.

JEDWALI

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 10(1))*

KUFILILISHA KOSA

Mimi…………………………………………. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………………………ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, kwamba mnamo tarehe ………mwezi………. Mwaka………. nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha………………. cha Sheria Ndogo ya Kudhibiti Ombaomba ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya ya mwaka 2021.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halamashauri ya Wilaya ya Chunya, Niko tayari kulipa kiasi ninayodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI KWELI NA NINAYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe………………………………. ya Mwezi…………………. Mwaka…………………

Jina…………………………………………Saini………………………………………

Mbele ya:

Jina………………………………………...Cheo…………………………………….

Saini………………………………………Tarehe……………………………………

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Chunya imebandikwa kwenye Sheria ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 30/6/2020:-

SOPHIA JUMA KUMBULI,
*Mkurugenzi,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Chunya*

MHE. BOSCO SAID MWANGINDE,
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Chunya*

L.S

NAKUBALI,

Dodoma,
22 Februari, 2021

SELEMANI SAID JAFO (MB.),
*Waziri wa Nchi -OR- Tamisemi*